

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA NNE

16 SEPTEMBER, 2022



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA NANE

KIKAO CHA NNE – TAREHE 16 SEPTEMBA, 2022

I. DUA:

II. HATIZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Maelezo ya Waziri wa Fedha na Mipango kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufuta Hasara/Upotevu wa Fedha na Vifaa vyta Serikali kwa kipindi kinachoishia Tarehe 30 Juni, 2022.



**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Kufuta Hasara/Upotevu wa Fedha na Vifaa vyta Serikali kwa kipindi kinachoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA WAZIRI MKUU:**

##### **48. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itaridhia Mkataba Na.189 wa Kazi za Staha kwa Wafanyakazi wa Majumbani.

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

##### **49. MHESHIMIWA JACKSON GEDION KISWAGA (KALENGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za kujenga Vituo vya Afya katika Kata ya Lyamzungwe na Kihanga.

##### **50. MHESHIMIWA LEAH JEREMIAH KOMANYA (MEATU):**


Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Maboma ya Zahanati Vijiji vya Lata, Ikigijo, Lukale, Malwilo, Bulyanaga, Shushuni, Nata, Usiulize na Igushilu yatakamilika.


**51. MHESHIMIWA ANTON ALBERT MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo ya Zahanati ya Ukoma kuwa Kituo cha Afya cha Kata ya Kisondela Wilayani Rungwe.



**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**



**52. MHESHIMIWA ZUBERI MOHAMED KUCHAUKA (LIWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, ni lini Serikali itafanya mapitio ya upimaji Vijiji nchini kwa kuwa migogoro mingi imesababishwa na upimaji usio shirikishi wa Mwaka 1970.

## **WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

### **53. MHESHIMIWA SHABAN OMARI SHEKILINDI (LUSHOTO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, ni lini Serikali itajenga uwanja wa Michezo katika Mji wa Lushoto.



## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **54. MHESHIMIWA TABASAMU HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvubi:-

Je, ni lini ujenzi wa banda la ukaguzi na kupokea samaki wabichi katika Kata ya Chifumfu utakamilika.

## **WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

### **55. MHESHIMIWA BONIPHACE MWITA GETERE (BUNDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, ni fursa zipi anazopata Askari anayeo a au kuolewa na Askari mwenzake.

## **WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:**

### **56. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, ni zipi sababu za Kiwanda cha Pamba na Mafuta cha Kasamwa kusimamisha uzalishaji kwa muda mrefu.

## **WIZARA YA MADINI:**

- 57. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina taarifa juu ya madini yanayopatikana Kakonko na Wananchi wanufaikaje.

## **WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

- 58. MHESHIMIWA ZAINABU ATHUMANI KATIMBA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni lini Serikali itaondoa utaratibu wa biashara mpya kutakiwa kulipa kodi ya mapato kabla ya biashara kuanza.

- 59. MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, ni hatua gani zitachukuliwa kwa walipa kodi walioshindwa kulipa na kuwa na malimbikizo makubwa lakini wapo tayari kulipa.

## **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:**

### **60. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-



Je, ni lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege wa Omukajunguti.

### **61. MHESHIMIWA HUSSEIN NASSOR AMAR (NYANG'HWALE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Barabara ya Kahama – Nyang'hwale – Busisi hadi Sengerema itajengwa kwa kiwango cha lami.

**62. MHESHIMIWA KABULA ENOCK SHITOBELA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Bandari zilizopo Mkoa wa Mwanza.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**63. MHESHIMIWA JESCA JONATHAN MSAMBATAVANGU (IRINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ipo tayari kuanzisha Shule maalum Kikanda ili kusaidia Watoto walioathirika na ukatili wa kijinsia.

## **WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

- 64. MHESHIMIWA COSATO DAVID CHUMI (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inaweza kuongeza uhai wa paspoti za muda wanazopewa Madereva hadi kufikia Miezi sita.



## **WIZARA YA MAJI:**

- 65. MHESHIMIWA SHALLY JOSEPHA RAYMOND (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni programu zippi zinatekelezwa kuvuna maji ya mvua na asilimia ngapi ya Wananchi hutumia huduma hiyo.

## **WIZARA YA KILIMO:**

- 66. MHESHIMIWA DANIEL AWACK TLEMAI (KARATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha miundombinu ya Skimu ya maji katika Kijiji cha Mbuganyekundu.

**67. MHESHIMIWA SOUD MOHAMMED JUMAH  
(DONGE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mpango gani kuboresha *The National Herbarium of Tanzania* Arusha ili kuimarisha huduma za utafiti na uhifadhi wa Mimea nchini.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**MAAZIMIO:**



**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Azimio la Bunge la Kuridhia Kufuta Hasara/Upotevu wa Fedha na Vifaa vyaa Serikali kwa kipindi kinachoishia Tarehe 30 Juni, 2022.

**DODOMA  
16 SEPTEMBER, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**